JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKINOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI LULUMBA,
S. L. P. 08,
KIOMBOI – SINGIDA,
SIMU: 0787439490/0712337779

Ndugu ……..

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018

1.0. UTANGULIZI

Napenda kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule ya sekondari LULUMBA, Hongera sana. Hii imetokana na bidii na juhudi zako ulizozionesha katika masomo yako ya kidato cha kwanza hadi cha nne.

Shule ya sekondari LULUMBA ni shule yenye wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita, ni shule ya kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne na ni shule ya wasichana na wavulana kwa kidato cha kwanza hadi cha nne. Tunakukaribisha sana ili upate elimu bora.

Aidha nafasi uliyoipata ni ya kujivunia na unatakiwa kuitumia vema kwa manufaa yako, familia na taifa kwa ujumla. Kumbuka, '**elimu ni ufunguo wa maisha'** itafute kwa bidii. Kiwango cha ubora wa maisha ya usoni kwa kila mtanzania na taifa kinategemea maandalizi yako ya sasa katika elimu bora ili kuikwamua jamii hususani familia yako inayowekeza katika **ELIMU BORA NA ENDELEVU** katika janga la ujinga na umasikini.

1**:1 KAULI MBIU, DIRA, DHAMIRA NA WIMBO WA SHULE**

1:1.1 KAULI MBIU (MOTTO)

- Kauli mbiu ya shule ni elimu hushinda vyote *"EDUCATION CONQUERS ALL "*

1:1.2 DIRA (VISION)

- Dira ya shule yetu ni – kutoa elimu bora ili kuendeleza jamii yetu

"PROVISION OF QUALITY EDUCATION IN ORDER TO DEVELOP OUR SOCIETY"

1:1.3 DHAMIRA (MISSION)

- Dhamira ya shule hii ni kuwa, kila mwanafunzi lazima apate elimu bora

"EVERY STUDENT SHOULD ACHIEVE QUALITY EDUCATION"

1:1. 4 WIMBO WA SHULE.

- Lulumba sekondari inao wimbo ambao kila mwanafunzi anapaswa aufahamu.
- Yafuatayo ni maneno ya wimbo huo.

1. *Lulumba yetu shule ya sekondari, ninaipenda kwa moyo wangu wote.*
   Mandhari yake yanavutia sana, elimu pia motomoto.
   Chorus Elimu ndiyo motto wa shule yetu, Nidhamu ndiyo ngao yetu, muungano pamoja na mashauri, utu, umoja na upendo.
2. *Shule yetu ina walimu wazuri, wenye ujuzi mwingi wa kufundisha, wanafunzi pia tunawajibika, masomo ndio ngao yetu.*
3. *Shule iliko ni Wilaya Iramba, mashariki mwa mji wa Misigirii, imepambwa kwa miti nayo maua, ukipita utaiona.*

2.0 MASOMO YANAYOFUNDISHWA

- Shule ni ya mchepuo wa sayansi tu kwa combination za PCM na PCB. Hivyo, masomo yanayofundishwa ni pamoja na Physics, Chemistry, Biology, Advanced mathematics, Basic applied mathematics na General studies.

3.0 MAHALI SHULE ILIPO

- Shule ipo katika makao makuu ya Wilaya ya Iramba (Kiomboi) Mkoa wa Singida Ukifika MISIGIRI kutokea Nzega au Singida utapata usafiri wa moja kwa moja hadi Kiomboi, Shule ipo katikati ya Kiomboi Bomani na Old Kiomboi. Ipo kwenye mandhari nzuri, Maua, Miti ya matunda na kadhalika huiweka shule kwenye mazingira ya kupendeza.

4.0 KUFUNGUA SHULE

- Shule itafunguliwa tarehe …… njoo mapema siku hiyo. Unatakiwa kuwepo kuanzia saa11: jioni. (Kama utapata udhuru wa kutokufika siku hiyo, wasiliana kwa namba za simu zilizopo hapo juu).

4.1 OFISI UTAKAZOPOKELEWA

- Ukifika shuleni nenda moja kwa moja kwenye ofisi ya Makamu Mkuu wa shule ambako utapokelewa na kusajiliwa. Aidha utatakiwa kwenda ofisi ya mhasibu kwa

ajili ya malipo ya ada na michango mingine ya shule kama ilivyoainishwa kwenye mahitaji ya shule

5.0 MAHITAJI YA SHULE

5.1 ADA NA MICHANGO YA SHULE

5.1. 1.**Ada**

- Ada ya shule ni Tsh. 70,000/= kwa mwaka. Unaweza kulipa yote au awamu mbili, Lipa ada na hakikisha unapewa risiti. Mwanafunzi atakayefika shuleni bila ada hatasajiliwa.

5.1.2. Mchango wa Taaluma Tsh. 10,000/=

5.1.3. Fedha ya dhamana / Tahadhari Tsh, 5,000/= (Hairudishwi)

5.1.4. Mchango wa mlinzi Tsh 10,000/=

5.1.5. Mchango wa madawati Tsh 15,000/=

5.1.6. Mchango wa wapishi Tsh 20,000/=

5.1.7. Mchango wa ukarabati Tsh 30,000/=

5.1.8. Kitambulisho Tsh. 5,000/=

5.2 MAHITAJI YA TAALUMA

5.2.1. RIMU MOJA A-4 na siyo aina nyingine pia lisifunguliwe na kupunguza karatasi (utaleta kila mwaka)

5.2.2. Jalada /file jipya lenye kamba kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zako.

5.2.3. Vitabu vinavyoendana na combination yako (vitabu vilivyo kwenye maktaba ya shule havikidhi mahitaji ya kila mwanafunzi)

5.2.4. Madaftari yanayotosheleza matumizi yako kwa mwaka mzima

5.3 MAHITAJI YA VIFAA VYA USAFI, MALAZI NA CHAKULA

5.3.1. Mfagio wa sakafu mmoja (soft bloom)

5.3.2. Ndoo ndogo moja

5.3.3. Sahani 1, bakuli 1 kikombe 1, na kijiko 1.

5.3.4. Mashuka 2 rangi ya bluu bahari, blanketi 1 (kuna baridi Iramba) na taulo

5.3.5 Godoro 1.(2.5’ x 6’ x 4’’)

5.1.9 CHF Tshs. 1,000/=

5.1.10 Mchango wa mahafali = 10,000/= kwa mwaka

5.4 SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORMS)

5.4.1.

Mwanafunzi anapaswa kuja na suruali 2 za bluu bahari (Light blue) zisizo za kubana (chini iwe inchi 14' au 15'), tai 2 rangi ya bluu bahari, mashati 2 ya mikono mirefu (yatakuja kuwekwa nembo ya shule), sweta 1 rangi ya bluu bahari. Tsh 12,000/= kwa ajili ya T-shirt ya shule (T-shirt nzito ya njano yenye kola na nembo ya shule)

5.4.2.

Viatu vya ngozi rangi nyeusi vinavyofunika miguu vyenye kamba na soli ni ya kawaida na sio vinginevyo.

5.4.3. Jozi mbili soksi nyeusi (STOCKINGS)

5.4.4. Nguo za michezo, bukta, T-shirt rangi ya kijivu isiyo na maandishi na raba.

5.4.5. Shamba dress (T-shirt dark blue).

6.0 TAALUMA.

- Shule hii inajali sana taaluma bora kwa wanafunzi wote. Hivyo mwanafunzi aliyechaguliwa kuja LULUMBA ni bahati na atatakiwa kusoma kwa bidii zote na kuachana na tabia zitakazomuathiri kimasomo ili aweze ili aweze kufaulu vizuri masomo yake. Shule haiwavumilii kabisa wanafunzi wanaotoroka darasani. Utaratibu wa wiki nzima (school routine) Utatolewa na kukupa fursa ya kufuata kwa ukamilifu ratiba ya shule. Aidha kutokufanya mtihani au jaribio ni kosa linaloweza kumsababishia mwanafunzi kupoteza nafasi yake ya kuwa shuleni.

7.0 HESHIMA, ADABU, UTII NA SHERIA ZA SHULE

- Mwanafunzi uliyepata nafasi ya kujiunga na shule hii huna budi kuwa na adabu, utii na heshima kwa walimu wako, watumishi wengine, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla. Mwanafunzi atakayebainika kutokuwa na tabia njema, au kuwa jeuri **ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA**. Aidha mzazi atatakiwa amwonye mwanae na kumtahadharisha na tabia za kutokufuata sheria za

shule na kufuata mkumbo. Tabia za mapenzi zinampotezea mwanafunzi muda, hivyo haviruhusiwi na anayekamatwa akijihusisha na tabia hizo hatavumiliwa shuleni. ***Matumizi ya simu za mikononi shuleni hayaruhusiwi kabisa kwa mwanafunzi hivyo tunakushauri mzazi usimnunulie mtoto wako simu ama usimruhusu aje na simu shuleni.***

- Zifuatazo ni SHERIA ZA SHULE zinazotakiwa kuzingatiwa na mwanafunzi siku zote awapo shuleni na mahali pengine popote nje ya shule:

1. Simu za mkononi haziruhusiwi kabisa shuleni; mwanafunzi akikamatwa na simu shuleni atafukuzwa shule mara moja.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kutoroka shule. Akitoroka shule na kuonekana nje ya shule bila ruhusa atafukuzwa shule mara moja.
3.
4. Mwanafunzi asipohudhuria masomo darasani na maandalizi ya usiku "NIGHT PREPARATION" atasimamishwa masomo wiki zisizopungua tatu au zaidi.
5. iv) Mwanafunzi akigomea adhabu atafukuzwa shule.
6. Mwanafunzi akichelewa kuripoti shuleni akitokea likizo atarudishwa nyumbani kumfuata mzazi wake ili aeleze sababu za kuchelewa kufika shule kwa wakati. Kama sababu za mzazi hazitajitoshereza, mwanafunzi atapewa adhabu stahiki kwa kuzingatia maoni ya ofisi ya nidhamu.

- Makosa mengine yanayoweza kusababisha mwanafunzi afukuzwe shule ni pamoja na:-

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
4. Kupigana au kupiga.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
6. Kudharau bendera ya taifa.
7. Kuoa au kuolewa.
8. Kupata au kusababisha mimba nakutoa au kushiriki kutoa mimba.

9. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu na
10. Kulala nje ya shule.

7.0 UTARATIBU WA KULIPA FEDHA

- Fedha zote za ada na michango mingine zitalipwa **BANKI ya NMB** akaunti namba **5061100137**, jina la akaunti ni **LULUMBA SEC.CAPITATION GRANT**. Mzazi /Mlezi atatakiwa kumlipia mwanafunzi ada na michango mingine kabla ya kuripoti shuleni. Njoo na**pay – in – slip** siku ya kuripoti, hakikisha unaandika jina kamili la mwanafunzi kwenye **pay-in-slip** hiyo.
- NB: Hatutapokea mwanafunzi atakayekuja bila malipo hayo. Kama kuna taarifa zingine kuhusu malipo tafadhali njoo nayo ikiwa na mhuri wa ofisi itakayohusika na malipo yako.

TUNAKUTAKIA SAFARI NJEMA

……

YEREMIA M. KITIKU

MKUU WA SHULE

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATION TRAINING
PRESIDENT'S OFFICE – RALG
LULUMBA SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 08,
KIOMBOI,
DATE……..

To the medical officer,
……..
Dear Sir/Madam

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:-

Please examine Mr/Miss
…… As to his/her fitness as a full time (student of this school) may I kindly requests you to fill in the particulars given in the form here under.
(Yours Sincerely).
……
The Headmaster
……

TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER

1. Blood count(White blood cells)…….
2. Stool examination……
3. Urine examination……
4. Gestation (for girls only)…….
5. Venereal diseases…….
6. T.B test……
7. E.N.T problem…….
8. Defects of (a) The left and right eye……..
   (b) The Chest……
9. Does he/she has any CHRONIC disease eg. Epilepsy cell, Anemia, Athma etc.

……
….....
I have examined Mr/Miss ……. And certify that he/she is physically fit to persue studies as stated above

……
Name and Signature of the medical officer

Date……
Designation……..